# MWONGOZO WA MSAIDIZI WA MWALIMU KWA WANAFUNZI VIZIWI WASIOONA KATIKA DARASA JUMUISHI

**2017**

# Sehemu ya kwanza

## Utangulizi

### Usuli

Mwongozo huu umeandaliwa kukidhi mahitaji ya msaidizi wa mwalimu katika kumjengea uwezo wa kufundisha wanafunzi viziwiwasioona katika darasa jumuishi. Pia utasaidia wasaidizi wa walimu kutoa msaada wa moja kwa moja kwa wanafunzi viziwiwaasioona katika kipindi chote cha ujifunzaji wao darasani. Aidha mwongozo huu umefafanua dhana, chanzo na aina za ukiziwikutoona. Vilevile unamwelekeza msaidizi wa mwalimu ufundishaji katika darasa la awali, la kwanza na la pili kwa kuzingatia mbinu na njia za ufundishaji. kwa wanafunzi hao.

### Dhana ya ukiziwi kutoona

Ni mtu yeyote ambaye ana ulemavu wa kutoona na kusikia kwa pamoja na wakati mwingine anaweza kuwa na ulemavu mwingine kama vile ulemavu wa akili au viungo. Ulemavu huu humfanya mtu ashindwe kuwasiliana vizuri na kumudu mazingira aliyomo.

### Vyanzo cha ukiziwikutoona

Ukiziwikutoona unaweza kumpata mtu kabla au baada ya kuzaliwa. Vyanzo vya ukiziwikutoona vimegawanyika katika sehemu kuu tatu:

a) **Kabla ya kuzaliwa:-** Mtu anaweza kuzaliwa na ulemavu wa ukiziwikutoona kutokana na sababu mbalimbali kwa mfano, mama mjamzito anapougua surua (kwa kitaalamu ugonjwa wa Rubella au German measles), au magonjwa ya zinaa kama vile kisonono na kaswende. Wakati mwingine matatizo yoyote wakati wa ujazito mfano, lishe duni,ajali, au mama mjamzito anapotumia madawa ya kulevya au dawa kali bila ushauri wa daktari, vileo, sigara na vipodozi vikali. Pia ulemavu huu mtoto anaweza kurithi kutoka kwa wazazi au anapozaliwa na wazazi wenye umri mkubwa.

b) **Wakati wa kuzaliwa:-** Ukiziwikutoona unaweza kutokea wakati mama anapojifungua kisha mtoto akapata matatizo ya kukosa hewa safi (oxygen) mapema (mtoto kutolia kwa wakati) na kusababisha eneo la ubongo unaohusisha usikivu kuathirika. Mama akipata ajali au kupata uchungu wa muda mrefu bila kujifungua

inaweza kusababisha mtoto kupatwa na ukiziwikutoona. Vilevile mtoto akizaliwa kwa njia ya kuvutwa na mashine huweza kusababisha ukiziwikutoona.

c) **Baada ya kuzaliwa:-** Milango ya fahamu ya uoni na usikivu inaweza kuathiriwa na magonjwa mbalimbali, hivyo kumsababishia mtu ukiziwikutoona. Sababu nyingine ni kupata ajali inayoweza kusababisha ukiziwikutoona. Vile vile lishe duni, homa kali, ugonjwa wa uti wa mgongo unaweza kumsababishia mtu ukiziwikutoona. Hata hivyo wataalamu wanasema kuna sababu zingine zisizojulikana kitaalamu zinazosababisha ukiziwikutoona (unknown causes).

## Aina ya ukiziwikutoona

I. Kiziwi ndi asiyeona kabisa
II. Mwenye baki ya usikivu na uoni hafifu
III. Kiziwi ndi mwenye uoni hafifu
IV. Mwenye baki ya usikivu asiyeona kabisa
V. Kiziwiasiyeona mwenye ulemavu mwingine

## Malengo ya Mwongozo

Mwongozo huu unalenga:

a. Kumwelekeza msaidizi wa mwalimu mbinu na njia mbalimbali za kuwasaidia watoto viziwiwasioona katika ujifunzaji.
b. Kumjengea msaidizi wa mwalimu uwezo wa kufundisha stadi wezeshi kwa watoto viziwiwasioona.
c. Kumwelekeza msaidizi wa mwalimu upimaji wa awali wa mtoto na kutumia mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi (Individualized Education Programme- I.E.P).

## Walengwa wa mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa mahsusi kwa ajili ya wasaidizi wa walimu pamoja na watoto viziwiwasioona. Pia unaweza kutumiwa na walimu, wazazi, walezi, na wadau wengine wa elimu mfano Maafisa elimu, waratibu elimu Kata, wakuza mitaala wathibiti ubora wa shule na taasisi zinazosaidia utoaji elimu kwa wanafunzi viziwiwasioona.

## Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu una sehemu kuu nne muhimu zifuatazo:-

a. Taarifa za awali
b. Ufundishaji wa darasa la awali,
c. Ufundishaji wa darasa la kwanza na

d. Ufundishaji wa darasa la pili.

Unashauriwa kufuata maelekezo katika mwongozo kwa kuzingatia aina ya ulemavu wa mtoto,aidha kama ana baki ya usikivu au uoni hafifu, hakikisha unatumia vema uwezo alionao ili apate kufaidika na elimu inayotolewa kwake katika ngazi zifuatazo:

# Sehemu ya pili

## Ufundushaji darasa la awali

Katika darasa la awali mtoto anakuwa hajapata uzoefu wa kushirikiana na watu zaidi ya wale waliopo katika familia yake nyumbani. Ni jukumu lako msaidizi wa mwalimu kufanya uchunguzi au upimaji wa awali ili kubaini masuala muhimu kuhusu mwanafunzi wako. Kwa mfano:

a. Tafuta historia ya mtoto kwa kutumia taarifa kutoka ka wazazi na mwalimu wa darasa. Hii itakusaidia kuelewa yale masuala muhimu kuhusu mtoto.
b. Hakikisha usalama wa mtoto ili awe huru kujifunza. Mruhusu kutumia milango yote ya fahamu ili aweze kugundua watu au vitu vinavyomzunguka (kunusa, kugusa , kupapasa na kuhisi.
c. Tumia vifaa mbalimbali kuchunguza uwezo wa mtoto wa kuona kwa mfano:
    - Vitu vyenye rangi mbalimbali zinazowaka - nyekundu, bluu na manjano.
    - Rangi za kawaida (neutral colours) kama - nyeupe, nyeusi, maziwa na kijivu.
    - Rangi hafifu kama - kijani, zambarau na machungwa.
d. Tumia vifaa mbalimbali vinavyotoa sauti kuchunguza uwezo wa mtoto wa kusikia kwa mfano; filimbi, ngoma, marimba na vingine kutoka katika mazingira ya shule.
e. Unashauriwa kuwashirikisha mwalimu wa darasa , mzazi na mwalimu mtaalamu wa viziwiwasioona na wataalamu wengine kama wapo (afya na ustawi wa jamii) kumwandalia mtoto mpango binafsi wa elimu wa kujifunza ((I.E.P). Mpango huu utakusaidia kubaini uwezo wa mtoto wa kupokea maarifa na jinsi maendeleo yake yanavyobadilika katika kipindi chote cha ujifunzaji.
f. Msaidizi wa mwalimu ufanye upimaji endelezi kwa kutumia orodha hakiki (checklist) ili kuweka kumbukumbu ya mambo ambayo mtoto tayari ameweza na yale ambayo utamsisitizia katika kujifunza. Kumbuka kumpongeza mtoto katika kila anachojaribu kufanya.
g. Hakikisha unazingatia suala la kumudu darasa kwa kutekeleza mambo yote muhimu kama vile:
    - kuzingatia ratiba

- kumchagulia mwanafunzi nafasi ya kukaa kulingana na tatizo lake- asihamehame sehemu ya kukaa darasani.
- Kujenga mahusiano mazuri na mtoto kwa kuzingatia mawasiliano mazuri pia kumjengea uwezo wa kujiamini, kushirikiana na wanafunzi wenzake na mwalimu.

Katika darasa la awali kuna stadi sita kama zilivyoelezwa hapo chini kwa mtiririko: Kumbuka kuzingatia aina ya ulemavu wa mtoto na uwezo alionao katika kujifunza. Anza na vitu rahisi na nyepesi kwa mtoto kuelewa.

## Kuwasiliana

Mwalimu unatakiwa umshirikishe mwanafunzi kutambua vigezo vya mawasiliano mfano; kugusa, kunusa, kupapasa,kutoa sauti, kunyoosha mikono kupokea au kukataa.
Tumia lugha ya alama-mguso au njia yoyote anayotumia mtoto kuonyesha kujitambulisha, kutambuana na kusalimiana katika sehemu mbalimbali kama vile:

- Nyumbani; baba, mama, dada, kaka, babu, bibi,
- Shuleni, shikamoo mwalimu, hodi, karibu
- Tabia na mwenendo– pole, asante, ndio, hapana, ninaumwa, habari, nzuri.

## Kutunza Afya ya Binadamu

a) Usafi wa mwili - mwelekeze mtoto kufanya usafi wa mwili. kwa mfano kunawa mikono kwa sabuni, kupiga mswaki, kunawa uso, kutumia dawa ya meno, kuchana nywele kwa chanuo au kitana. Kutofautisha maji baridi / moto, barafu, upepo, joto n.k
b) Usafi wa nguo - mwongoze mtoto kubainisha nguo na kufanya usafi mfano; nguo za ndani, soksi, shati, sketi, kaptula, fulana, pia vifaa vya kutumia kufulia, kupiga pasi.
c) Vyakula - Maji, matunda, chakula, mboga, kupika, kula, chumvi, sukari.

## Kutunza mazingira

Mwelekeze mtoto kutambua mazingira yanayomzunguka na vitendo vya kufanya usafi kulingana na mahali kwa mfano;

a) Shuleni;
    - Darasani: Kufagia, kuzoa taka, kufuta vumbi na kupanga vitu.
    - Nje ya darasa: matumizi sahihi ya choo, kupanda maua, kumwagilia bustani, kuokota taka, kuzoa taka na zoleo, kutupa taka seheumu iliyo sahihi.

b) Nyumbani: Mtoto aelekezwe vyumba, madirisha, milango, choo, jiko, na vyombo vinavyotumika. Ajengewe uwezo wa kufuata ratiba ya kuamka asubuhi na *ratiba* ya chakula mchana na jioni.

c) Mtaani: Mtoto aelekezwe mara kwa mara mazoezi ya utambuzi wa sehemu muhimu jirani na nyumbani kama vile dukani, gengeni , bomba la maji lilipo, kanisani na msikiti. Ni muhimu mtoto aelekezwe kununua vitu dukani na gengeni, pia matumizi ya hela na kujengewa uwezo wa kutambua kurudishiwa chenji kwa usahihi.

## Kumudu Utendaji wa Mwili

Matendo ya kawaida:

a) Mwelekeze mtoto matumizi sahihi ya chooni. Kujinawisha mwenyewe baada ya kujisaidia au kutumia karatasi laini (toilet paper) pia kunawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka chooni.

b) Mtoto aelekezwe kutofautisha vitu vizito na vyepesi , vimiminika na vigumu (Mfano mafuta ya maji na ya mgando) vilevile vitu laini, vigumu na vya kukwaruza kama msasa kwa kugusa na kunusa.

c) Mwonyeshe mtoto kwa vitendo kuruka, kukimbia, kucheza, kubembea, kutembea, kusimama, kukaa kuimba, kulala, pia kushikana mikono katika duara, kupeana (kupasiana) au kurushiana vitu kama mpira au mifuko ya mbegu.

*d)* Maelekezo: tumia njia mbalimbali za kumshirikisha mtoto kutambua matendo mbalimbali ya hisia kwa mfano; kucheka, kulia, kasirika, sikitika, vilevile mtoto aweze kutambua maelekezo kama nenda/rudi, leta/peleka, acha, kataa, funga/fungua.

*e)* Vionjo: Mara nyingi mtoto kiziwiasiyeona hunusa vitu kabla ya kuonja. Mwelekeze kutofautisha vitu vitamu, sukari, asali, chumvi, chungu, kali, pilipili, ukwaju, ndimu, limau na dawa.

## Kumudu Stadi za kisanii

Katika kujifunza stadi za kisanii mwelekeze mtoto kulingana na uwezo wake wa kiutendaji pia kwa kuzingatia kile anachopenda na anaweza kumudu kufanya. Kuchora, kufinyanga, kuumba, kusokota kupamba, kupaka rangi, kusuka na kucheza ngoma.

## Kutambua stadi za kuhesabu

a. Tumia vitu halisi na zana za kuhesabia kama kadi za namba.Toa maelekezo kwa lugha ya alama, alama mguso na vitendo. Katika ngazi hii ya elimu ya awali mtoto anatakiwa aelekezwe pia kutambua seli za Breli.

b. Kwa kutumia njia shirikishi za vitendo, michezo na kuimba mfundishe mtoto alama za namba 1-10. mfano, kutembea kwa hatua moja, mbili – hadi tano; pia kuendeleza hadi 10, kuruka, kupiga makofi, kutumia mawe, vijiti, mbegu, visoda na kadi za namba-mguso.

c. Hakikisha unamwelekeza mtoto alama ya namba husika mpaka awe ameiweza vizuri kabla hujamwanzishia namba zingine.

# Sehemu ya tatu

## Ufundishaji darasa la kwanza

### Stadi za Kusoma - Msaidizi wa mwalimu, mwelekeze mwanafunzi

a) jinsi ya kuumba herufi **a** kwenye mdomo, kwenye mkono kwa alama- mguso na kutambua doti kwa kutumia kibao cha seli.
b) kuimba herufi aaaaaaa kwa kutumia lugha ya alama
c) jinsi ya kutamka **a** kwa kugusa chini ya taya ili kusikia mtetemo
d) alama za kila irabu kwa nukta nundu kumwezesha mwanafunzi kutambua irabu a, e, i, o, u.
e) Kusoma irabu a, e, i, o, u kwa kutumia tahajia ya vidole (finger spelling)
f) Kuumba herufi za konsonanti baada ya kufuzu kutambua irabu.
g) Kujifunza silabi mfano ba, be, bi, bo,bu.

Zingatia uwezo wa mwanafunzi na mahitaji ya ujifunzaji kama atanufaika zaidi kwa lugha ya alama au Breli. Hakikisha maandishi yawe makubwa.

### Stadi za Kuandika

a) Mara nyingi mwanafunzi kiziwiasiyeona mwenye uoni hafifu ndiye anaweza kunufaika kupata stadi za kuandika bila breli. Maandishi sharti yawe makubwa. Kwa wale wasioona waelekezwe matumizi ya nukta nundu na breli.
b) Mwelekeze mwanafunzi kuandika michoro mbalimbali ya herufi za irabu na konsonanti hatua kwa hatua.
c) Mwelekeze jinsi ya kuchora maumbo mbalimbali hewani kabla ya herufi husika ili kumpatia mazoezi ya vidole
d) Mwanafunzi apewe mazoezi ya kutosha kuchora herufi aaaaa hewani kisha kwenye vibao vidogo. Mwalimu aelekeze mtoto kuandika maandishi makubwa ya herufi husika.

### Stadi za Kuhesabu

a) Mwanafunzi aweze kutambua namba 11 – 20 kwa kutamka na kuonyesha kwa lugha ya alama.
b) Kutambua idadi ya vitu kwa kuoanisha na namba kwa lugha ya alama mguso mfano: OOOOOOOOOOO= 11
c) Mwanafunzi aelekezwe kubaini majina ya namba kwa mfano: 1 = moja, 10 = kumi, 11 = kumi na moja
d) Kutambua alama za **+** na **-**

e) Kufundisha matendo ya kujumlisha kwa kutumia vihesabio idadi isiyozidi 20.na matendo ya kutoa idadi isiyozidi 20
f) Mchoro kuonesha dhana ya sifuri, Mwalimu utumie mifano halisi ili kufundisha dhana ya sifuri. Kwa mfano; mwonyeshe mtoto chupa yenye maji masafi kisha anywe maji yote, yakiisha unamwelekeza kuwa chupa imebaki tupu bila kitu ndani yake. N.k
g) Kutambua thamani ya fedha 50,100,200,500,1000 ( shilingi hamsini hadi Sh. Elfu moja) kwa kutumia picha- mguso na pesa halisi. Mwelekeze mwanafunzi kutambua na kutofautisha fedha za sarafu na noti. Unaweza kwenda naye dukani ili aweze kujifunza kununua na kurudishiwa chenji, pia kutambua thamani ya fedha kwa kununua vitu.
***h)*** Kutambua dhana ya kitu kizima na nusu. Mwelekeze mwanafunzi atambue chungwa zima kisha ulikate ili apate kutambua nusu. Tumia vitu tofauti ili mwanafunzi aweze kujenga dhana ya kitu kizima na nusu

## Stadi za Kutunza Afya na Mazingira

Mwelekeze mwanafunzi:

a) Atambue sehemu za mwili wake kwa mfano; kichwa, uso, macho, masikio, mdomo, meno nk.kwa lugha ya alama, ishara, alama mguso kwa kutumia michoro na vielelezo vya sehemu za nje za mwili wa binadamu.
b) Kutambua matumizi ya sehemu za mwili kwa mfano; macho hutumika kuona, masikio- kusikia, mdomo – kula, meno – kutafuna na pua – kunusa.
c) Mtoto ajifunze kwa kutumia vifaa na vitendo kuonesha usafi wa mwili.
d) Mtoto ajifunze kwa kutumia vifaa na vitendo kuonesha usafi wa mazingira kufua, kuanika, kuanua, kupiga deki.
e) Michoro ya aina mbalimbali ya vyakula na vinywaji, Mifano ioneshe picha pamoja na alfabeti

## Stadi za Sanaa na Michezo

a) Mwalimu amuelekeze mwanafunzi michezo kwa mfano mdako, kombolela, kuruka na kudaka mpira, nyama nyama nyama. kwa usahihi kwa kutumia vifaa mbalimbali vya michezo kama , kamba, mpira, kete za mdako na vifuko vya mbegu.
b) Kwa kutumia lugha ya alama na tahajia ya vidole mwalimu amwelekeze mtoto kuchora maumbo ya herufi, namba na vitu mbalimbali.

c) Kumwelekeza mwanafunzi kufinyanga, kupaka rangi, kusuka, kuimba nyimbo kwa kufuata mapigo ya ngoma.

# Sehemu ya nne

## Ufundishaji wa darasa la pili

### Stadi za Kusoma

a) Mwalimu unatakiwa kuanza somo kwa utangulizi mfupi wa habari kwa kuumuuliza mtoto kusimulia habari yoyote aliyonayo kutoka nyumbani. Hii ni kwa ajili ya kumuandaa kujifunza.

b) Tumia michoro ya alama za silabi na maneno kwa kutumia nukta nundu na mitetemo ya sauti.

c) Ziwekwe picha kuonesha umbo la mdomo wakati wa kutamka silabi, maneno na sentensi fupi kwa kutumia lugha ya alma.

d) Kioo kikubwa cha ukutani kitumike ili unapotamka mtoto aone na kufuata matamshi. Kwa wale ambao hawanufaiki kwa njia hiyo, mwalimu aelekeze jinsi ya kutumia lugha ya alama, nukta nundu na kupapasa.

e) Mwalimu amwongoze mwanafunzi kusoma silabi, neno, sentensi na habari fupi kwa kutumia lugha ya alama,alama mguso, kupapasa na nukta nundu.

### Stadi za Kuandika

a) Mwongoze mwanafunzi kukuza ujuzi kwa kuandika silabi, maneno, sentensi fupi na habari fupi.

b) Mwelekeze mwanafunzi kuandika herufi kubwa na ndogo kwa kutumia lugha ya alama na nukta nundu, pia kwa maandishi makubwa.

c) Kwa kutumia picha au kadi mwelekeze mwanafunzi kuandika sentensi fupi na habari fupi.

### Stadi za Kuhesabu

Mwongoze mwanafunzi:

a) Kuonesha mchoro wa kuhesabu kwa lugha ya alama namba 21- 50

b) Kujua tarakimu kuanzia 21 hadi 50

c) Kujumlisha ( +) na kutoa ( -) kuanzia namba 21 hadi 50

d) Kukuza dhana ya kitu kizima na sehemu ½, ¼.

e) Kujua vipimo vya ujazo kwa mfano chupa ya maji ujazo wa lita moja.

f) Kubaini maumbo mbalimbali mfano; mraba, mstatili na duara.

g) Kubaini na kutofautisha fedha shilingi 2,000; 5,000 na 10,000.

h) kupanga vitu vyenye maumbo mbalimbali (puzzles)

i) kubaini mchoro kuonesha dhana ya sifuri

## Stadi za Kutunza Afya na Mazingira

Stadi hizi zinamjenga mwanafunzi kiafya, kimwili, kiakili na kisaikolojia.Unashauriwa kumjengea mwanafunzi ujuzi wa kutunza afya na mazingira kulingana na uwezo wake wa kujifunza.

### A. Kutunza afya

Mwelekeze mwanafunzi:

a) Sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu kwa kutumia mchoro unaoonyesha viungo vya mwili mfano; sikio, macho, mdomo, pua, kichwa na shingo

b) Kazi za viungo mbalimbali vya nje ya mwili wa binadamu kwa mfano; macho- kuona/kutazama, masikio- kusikia, mdomo – kuongea, kula na pua – kunusa, kupumua, kutoa uchafu nje (kupenga kamasi).

c) Matumizi ya vifaa vya usafi wa mwili kwa mfano; mswaki, dawa ya meno, sabuni, ndoo, beseni, maji, brashi/ jiwe, dodoki na taulo

d) Kufanya usafi wa mwili
- Kusafisha kinywa na kunawa uso.
- Kuoga na kusafisha sehemu mbalimbali za mwili kwa makini hasa sehemu kama vile kwapani na sehemu za siri.
- kusafisha nywele kuchana /kusuka, kukata na kupaka mafuta.
- Kukata na kusafisha kucha.
- Kufua na kuanika nguo. Mfano, nguo za ndani, soksi, sare za shule.
- Kusafisha viatu na kuvibrashi.

e) Kubainisha maambukizi ya magonjwa kwa mfano:
- Kuhara, kutapika, kipindupindu, tumbo - unasababishwa na kunywa maji yasiyo salama, vyakula visivyo safi, mfano, matundo yasiyosafishwa na kula ovyo ovyo sehemu zisizo safi kwenye magenge.
- Kichocho - kutokana na kutovaa viatu na kuoga kwenye madimbwi yenye maji machafu.
- Maambukizi katika njia ya mkojo (U.T.I), matumizi ya vyoo vichafu, uchafu wa nguo za ndani kama hazikauki vizuri, kutonawa vizuri baada ya kujisaidia.
- Malaria - kulala bila chandarua.

f) Mchoro wa kisanduku cha huduma ya kwanza - mwanafunzi aweze kubainisha vifaa vilivyomo kwenye kisanduku na matumizi yake kama vile:
- Pamba- kwa ajili ya kupaka dawa, kufuta damu/usaha pia uchafu kwenye macho, pua na mdomoni
- Nyembe / mkasi – kwa ajili ya kukatia vitu mbalimbali
- Bandeji /plasta – kufunga vidonda
- Dawa kama spirit – kusafishia michubuko na vidonda.

## B. Usafi wa Mazingira

Mwelekeze mwanafunzi:

a) Kusafisha choo kila siku kabla na baada ya kutumia.
b) Kutumia vifaa kama vile maji, brashi, fagio na ndoo.
c) Kulima bustani kwa kutumia vifaa mbalimbali kama jembe, panga na reki.
d) Kupanda mbegu za mboga, kumwagilia, kupalilia, kuvuna na jinsi ya kutumia mazao ya bustanini (kula na kuuza).

## Stadi za Sanaa na Michezo

Mwongoze mwanafunzi kujifunza kazi za sanaa pia michezo. Watoto hawa wana uwezo wa kutengeneza vitu mbalimbali vya kazi za mkono. Mwelekeze stadi zifuatazo na zingine utakazobuni kulingana na mazingira ya shule.

a) Kufinyanga maumbo ya vitu mbalimbali (mfano wanyama, vyombo, namba, herufi )
b) Kupaka picha rangi
c) Kuchapa unamu kwa kusugua na kugandamiza
d) Kusuka ukili
e) Kuimba na kuigiza.

Michezo:

Mwelekeze mwanafunzi michezo ya asili pia michezo mbalimbali kama vile;

a) kombolela, rede, mdako
b) kumrushia mpira na kumfundisha kudaka
c) Kurushiana vifuko vya mbegu
d) sarakasi rede, mdako
e) kuvuta kamba
f) kuzungusha ringi kwa kutumia kiuno

# Rejea


1. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2015), Mwongozo elekezi wa kubaini mahitaji ya ujifunzaji stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (kkk) kwa watoto, Wyemu, Dar es salaam
2. Taasisi ya Elimu Tanzania, (2006). mwongozo wa mwalimu wa kufundishia wanafunzi viziwi/wasioona katika shule za msingi Tanzania, Tet, Dar es salaam (Draft)
3. Taasisi ya Elimu Tanzania 2015 Najifunza michezo na sanaa darasa la kwanza Tet, Dar es salaam.
4. Taasisi ya Elimu Tanzania 2015 Najifunza kusoma darasa la kwanza Tet, Dar es salaam.
5. Tanzatoto Foundation 2014 kamusi ya lugha ya alama kwa watoto, tanzatoto foundation, Jan van gentlaan, heemstede, the Netherlands.